**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**686** **VITENDO VYA KUJIFUNZA KISWAHILI**

**Muda: Saa 3.** **Jumatatu, 02 Mei 2011**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**

2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.

3. Sehemu **A** ina alama **40** na sehemu **B** na **C** zina alama **30** kila moja.

4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.

5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Bainisha mbinu nne anazoweza kuzitumia mwalimu kumfundisha mtoto kuunda maneno kwa kutumia herufi au silabi.

2. Eleza kwa kifupi, jinsi gani mwalimu anaweza kutumia "muziki wa mwili" kuimarisha stadi ya kusikiliza kwa watoto.

3. Taja na fafanua kwa kifupi faida nne za kumfundisha mtoto kujibu maswali rahisi kwa sentensi fupi.

4. Chambua manufaa manne ya kutumia kadi za maneno zenye rangi mbalimbali katika ufundishaji wa kusoma.

5. Fafanua kwa kifupi mambo manne ambayo mwalimu anaweza kuyafanya ili kumfanya mtoto apende kusimulia hadithi.

6. Ainisha changamoto nne zinazoweza kumkabili mwalimu anayefundisha watoto wenye lugha ya mama inayotofautiana na Kiswahili.

7. Eleza kwa kifupi jinsi unavyoweza kutumia shughuli ya upishi rahisi (k.m., kutengeneza chapati) kufundisha lugha.

8. (a) Eleza maana ya 'usomaji shirikishi' (interactive reading).

   (b) Taja shughuli mbili ambazo zinaweza kufanywa wakati wa usomaji shirikishi.

9. Bainisha hatua nne za kufuata ili kumfundisha mtoto kutofautisha herufi 'b' na 'd'.

10. Kwa nini ni muhimu kwa mwalimu kuandika kwa hati inayosomeka vizuri? Toa sababu nne.

**SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali mawili (2) kutoka sehemu hii.

11. "Michezo ya nje ina mchango mkubwa katika ukuaji wa lugha." Thibitisha kauli hii kwa hoja tano.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

12. Fafanua kwa kina jinsi utakavyotumia mbinu ya hadithi-picha kumfundisha mtoto dhana ya mfululizo wa matukio.

13. Chambua faida tano za kutumia "kazi za mradi" katika ufundishaji wa stadi za kuandika kwa watoto.

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali mawili (2) kutoka sehemu hii.

14. Eleza hatua tano utakazozifuata ili kuandaa na kutumia tamthilia fupi darasani kwa madhumuni ya kukuza lugha.

15. "Mwalimu mbunifu anaweza kutumia taka kama zana bora za kufundishia." Jadili kauli hii kwa kutoa mifano mitano ya zana utakazotengeneza na jinsi zitakavyotumika.

16. Bainisha njia tano za upimaji wa maendeleo ya stadi ya kuzungumza kwa mtoto bila kutumia mtihani wa karatasi.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org